

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA SABA**

**KIKAO CHA ISHIRINI NA TISA**

**24 MEI, 2022**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA SABA


KIKAO CHA ISHIRINI NA TISA – TAREHE 24 MEI, 2022

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.



III. MASWALI:



OFISI YA WAZIRI MKUU:

248. MHESHIMIWA MIRAJI JUMANNE MTATURU  
(SINGIDA MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, ni lini Serikali itamaliza changamoto ya kuchelewesha Mafao kwa Wastaafu.

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**249. MHESHIMIWA CONSTANTINE JOHN  
KANYASU (GEITA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Mji wa Geita utakuwa Manispaa.

**250. MHESHIMIWA FLATEI GREGORY MASSAY  
(MBULU VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaongezea posho Madiwani na kuwalipa mishahara Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji.

**251. MHESHIMIWA INNOCENT SEBBA  
BILAKWATE (KYERWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaifungua Zahanati iliyopo Kijiji cha Nyakashengi Kata ya Businde ili iweze kutoa huduma kwa Wananchi.

**WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

**252. MHESHIMIWA ISSA JUMANNE MTEMVU (KIBAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

- Je, ni lini Serikali itajenga *Sport Arena* katika Wilaya ya Ubungo.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**253. MHESHIMIWA MWANTUM MZAMILI ZODO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Daraja la Bweni Wilayani Pangani.



**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**254. MHESHIMIWA AGNESTA LAMBERT KAIZA  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati Magereza ili kulinda haki za Wafungwa na Mahabusu.

**255. MHESHIMIWA TECLA MOHAMED UNGELE  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha Miundombinu ya Gereza la Liwale.

**WIZARA YA NISHATI:**

**256. MHESHIMIWA MICHAEL MWITA KEMBAKI  
(TARIME MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme kwenye Mitaa 61 katika Mji wa Tarime.

**WIZARA YA KILIMO:**

**257. MHESHIMIWA ALEKSIA ASIA KAMGUNA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha kilimo cha Mpunga katika Mkoa wa Morogoro.

**IV. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA  
24 MEI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**

